



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA ROMBO



(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

Simu namba: 027-2790008  
Fax Namba: 027-2757294  
Barua pepe: [ded@rombodc.go.tz](mailto:ded@rombodc.go.tz)

OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI,  
328 BARABARA YA SABASABA,  
S.L.P 52,  
25782 MKUU-ROMBO.

Unapojibu tafadhali taja:  
Kumbu. Na. HWR/S.40/28/87

29/12/2023

**TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA MKATABA**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rombo anatangaza nafasi za ajira ya muda ya kukusanya Ushuru/Mapato katika Halmashauri ya Wilaya ya Rombo.

**SIFA ZA MWOMBAJI**


- Awe amehitimu Elimu ya Kidato cha Nne/ Sita.
- Awe na Elimu ya Kuanzia Stashahada (Diploma) na Kuendelea kwenye fani ya Biashara/Uhas
- Awe tayari kufanya kazi sehemu yoyote atayopangiwa na Halmashauri.
- Awe Mkazi wa Rombo

**MAJUKUMU YA KAZI**

- Kukusanya Mapato.
- Kubaini vyanzo vya mapato.
- Kuwa kwenye kituo chake cha kazi wakati wote.

**MASHARITI YA JUMLA:**

- i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania wawe na umri kati ya miaka 18 hadi miaka 40.
- ii. Waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa.
- iii. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anwani na namo simu za kuaminika pamoja na majina yao.
- iv. Maombi yote yaambatane na cheti cha kidato cha nne, sita na vya taaluma
- v. Awe na kitambulisho cha mpiga kura, cha taifa au namba ya kitambulisho.
- vi. Picha mbili "Passport size" ya hivi karibuni iandikwe jina kwa nyuma.
- vii. Waombaji wenye ujuzi wa kutumia computer na wenye fani za udereva na wenye Pikipiki binafsi watapewa kipaombe zaidi.
- viii. Awe anaweza kutumia simu janja (smart phone).
- ix. Awe na wadhamini wawili.
- X. Maombi yote yawasilishwe masijala ya Mkurugenzi Mtendaji au kupitia barua pepe [ded@rombodc.go.tz](mailto:ded@rombodc.go.tz).
- x. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe **07/01/2024** saa **9:30** Alasiri.

  
Christina Marwa

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (HW),  
ROMBO**